# PAVEMENT FORM 4 TRIAL 2 EXAMINATION 2021/2022
## Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)
## 102/2

# LUGHA-JARIBIO LA PILI

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**UFAHAMU**

1. a .Teknolojia

b. Malipo ya kidigitali ni ya juu
- Teknolojia kutofikia kila mwananchi
- Kutokuwa na uwezo kumiliki simu ya kisasa yenye apu
- Ufisadi
- Kampuni kuondolewa kutoka soko la hisa

c. Kulinda matumizi

d.Vikwazo vikali kupitia kwa mamlaka ya ushindano (CAK)

e.Sera zafaa kuboreshwa ili kuvumisha ubunifu na kueneza hadhi mashinani

f. Mabadiliko

Kuwa na uwezo mkuu kwa kampuni moja

2. (a) **UFUPISHO**

(i)Ajira ya watoto ni tatizo sugu ulimwenguni.

(ii)Wengi huajiriwa katika nyanja mbalimbali.

(iii) Familia nyingi ni maskini (fukara)

(iv)Kupanda kwa gharama ya maisha huzidisha umasikini.

(v)Njaa huwatorosha nyumbani.

(vi)Ukimwi umezidisha mayatima.

(vii) Wengine hutoroshwa makwao na maonevu.

(viii) Wengine huondolewa shuleni.

(ix)Huko hutaabishwa kimwili na kiakili / hufanyishwa kazi za sulubu / hulipwa malipo duni au wasilipwe kabisa.

(x)Hili huwasononesha na kuathiri afya yao. **(al 6 1 ya mtiririko)**

(b)(i)Watoto wengine hujiingiza katika jinai wanapokosa ajira

(ii)Wengine hujikuta mandanguroni.

(iii) Uundaji wa umoja wa Afrika ni hatua ya kushughulikia matatizo barani.

(iv) Nchi za Afrika lazima zizingatie masharti ya umoja wa mataifa kuhusu watoto.

(v) Nyingi zaidhinisha watoto kupitia sheria zao.

(vi) Lazima zishughulikie watoto kupitia sheria zao.

(vii) Watoto ni rasilimali na tamaini la kizazi. **(alama 7 1 ya mtiririko.**

**Utuzaji**

**Sehemu a – 7**

**Sehemu b - 6**

**Utiririko alalma - 2**

**15**

**1.Adhabu – ondoa alama moja kwa kila ziada ya maneno 10 baada ya kumtuza**

**2.Ondoa alama ½ kwa kila kosa la hijai na sarufi (6h na 6s) baada ya kumtuza**

**3.Anayekosa kuandika matayarisho na jibu kwa haya moja asipewe alama za utiririko**



For free KCSE Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

**MATUMIZI YA LUGHA**

1.Andika maneno yenye miundo ifuatayo **(alama 2)**

(i) Kikwamizo hafifu cha ufizi,irabu ya mbele kati,nazali ya midomoni,irabu ya chini kati
**sema**

(ii) Nazali ya ufizi,Irabu ya juu mbele, kipasuo hafifu cha midomo,irabu ya nyuma kati
**nipo**

2 .Ainisha mofimu katika maneno yafuaatayo: **(alama 2)**

Asemavyo
**a-sem-a-vyo**
**a-mofimu tegemezi ya nafsi ya tatu umoja**
**sem-mzizi**
**a-kiishio**
**vyo-mofimu tegemezi ya -o -rejeshi tamati**

Mwangwi
**Mw-angwi**
**Mw-mofimu tegemezi ya umoja**
**Angwi-mzizi**

Teacher.co.ke

3.Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi wawili ya kiambishi `ni' **(alama 2)**

a) nafsi ya kwanza umoja
✓ **Ni**liwasili jana.

b) mahali
✓ Twende kanisa**ni**.

c) kitenzi kishirikishi kipungufu
✓ Yeye **ni** daktari.

d) wingi
✓ Toke**ni** nje.

e) Kama kiulizi wataka**ni?**

4. Ainisha vitenzi katika sentensi: **(alama 3)**

Ndege yu taabani, hata hivyo anajaribu kujinasua.
Yu-kitenzi kishirikishi kipungufu
Anajaribu-kitenzi kisaidizi
Kujinasua-kitenzi kikuu

5. Tunga sentensi ukitumia kirai kihusishi kama kielezi. **(alama 1)**

Mtoto ameanguka **chini ya meza.**

6.Unapoadhirika na jambo unasema hewala! Unaposhangilia timu yako kwa kupata ushindi unasema **hoyee/ huree/ hoyee/ oyee,/hario,/ripiripu.** unapotaka usikivu unasema **aisee/ ati/ebu,/hebu/ jamani, (alama 2**)

7.Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kinyume: **(alama 2)**

Wakimbizi walihama na wakavunja kambi .
**Wakimbizi waliishi na wakakita kambi**.

8.Tunga sentensi yenye muundo ufuatao **(alama 2)**

Nomino ya jamii, kirai kihusishi ,kitenzi kishirikishi,kielezo cha mahali.
**Kicha cha funguo ki mezani.**

9.Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Mtoto huyo mzuri alifika shuleni asubuhi na mapema.
**Mtoto huyo mzuri-kiima**
**Asubuhi na mapema-Chagizo**

10.Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Wachezaji walishinda mechi wakatuzwa.
**Wachezaji walishinda –Kishazi huru**



For free KCSE Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

**mechi wakatuzwa-Kishazi tegemezi**

11.Onyesha shamrisho ,kitondo, kiponzi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 3)**

**Mwanafunzi alimbebea mwalimu mzigo kwa gari.**

**mzigo-shamirisho kipozi**

**mwalimu-shamirisho kitondo**

**gari-shamirisho ala**

12.Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya A-WA **(alama 2)**

**M-WA**

**Mtu -Watu**

**M-MI**

**Mtume-Mitume**

**KI-VI**

**Kiwete-Viwete**

**CH-VY**

**Chura-Vyura**

13. Yakinisha sentensi ifuatayo katika nafsi ya pili umoja. **(alama 2)**

Hataenda shulenj kesho.

**Utaenda shuleni kesho.**

14. Eleza dhima ya tatu za viambishi tamati mbali na kauli ya kutenda/kiishio. **(alama 3)**

**Ukanusho – haji**

**Kauli ya kutendea – som- e- a**

**Undani/kielezi – darasa-ni / mahali asimama-po**

**Wingi / amrisho – amke-ni, cheze-ni**

**Unominishaji/uzoefu – ushona-ji**

**Kiendelezi – amk-e-ni**

**Wakati acheza-po** **(Za kwanza 3×1=03)**

15. Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali ya mazoea. **(alama 2)**

**Mwanafunzi alikuwa akisoma/asoma/anasoma kwa bidii shuleni.**

16. Changanua sentensi zifuatazo kwa kielezo cha mistari.

i) Huyu wake alikuwa amefika lakini hatukumjua. **(alama2)**

. **S-S1-KN(W+V)+KT(Ts+T)+U+S2-KN(O)+KT(T)**

ii) Mtoto wa Shangazi hucheka sana. **(alama 1)**

**S-KN(N+H+N)+KT(T+E)**

17. Eleza maana tatu zinazojitokeza katika sentensi. **(alama 3)**

Niliona Mamba.

**Mamba-aina ya Nyoka**

**Mamba-mnyama aishiye majini/Ngwena**

**Mamba-magamba ya samaki**

**Mamba-magome ya mti yaliyomeguliwa**

18. Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. **(alama 2)**

Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi.

**Vijidebe/videbe hivyo vitasafirishwa pamoja na vijinyundo hivi.**

**Ondoa makosa ya hijai na sarufi ipasavyo**

**ISIMU JAMII**

**Sajili ya matangazo ya biashara.**

(i) Lugha ya kuvutia hutumiwa, bidhaa moto moto ili kuvutia wateja.

(ii) Lugha shawishi mno hutumiwa, bidhaa nyororo sana ili kuwavutia wanunuzi.

(iii) Kuna matumizi ya takiriri bei rahisi, bei rahisi, bei rahisi, ili kusisitiza bei ya bidhaa.



For free KCSE Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(iv) Kuchanganya ndimi, bei ni affordable ili kuvutia wateja wengi.
(v) Athari za rangi hutumiwa ili kuvutia wateja wengi.
(vi) Athari za muziki hutumiwa, kuvutia wateja.
(vii) Huwa na ucheshi na porojo ili kuwavutia wateja.
(viii) Lugha isiyo sanifu hutumika ili kuwasilisha ujumbe kwa wote kwa urahisi.
(ix) Ubora wa bidhaa husisitizwa, ili kuwavutia wateja.
(x) Kuna upigaji chuku mwingi ili kuwavutia wateja.
(xi) Sentensi fupi fupi hutumika kurahisisha mawasiliano.
(xii) Kuna matumizi ya michoro kuvutia wateja.



For free KCSE Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/